Global Africa, Vol. 1, n° 1, p. 4 (2022)
DOI: 10.57832/ga.v1i1.15

GLOBAL AFRICA

Tahariri

Uhuru, ukweli, ujasiri !
Jarida la Umajumui wa Afrika kuhusu masuala ya utandawazi, hapa, na sasa.

Uhuru. Ukweli. Ujasiri ! Jarida la Umajumui wa Afrika kuhusu masuala ya utandawazi, *hapa, na sasa*

Vizazi vyote hukumbwa na athari ya mambo mageni ambayo hayajawahi kuwatokezea, lakini sisi Waafrika – ambao tuliingia kwenye karne 20 kabla ya sehemu yoyote na watu wowote wengine wa dunia, kupitia milango miwili tofauti kabisa ya uhuru na bumbuwazi; tunakabiliana na migogoro mikali ya kukosekana kwa usawa; kuzuka kwa mfululizo mambo yasiyotegemewa, lakini pia matumaini yanafifia huku matatizo ya zamani yakiwa bado hayajatatuliwa – hivyo tuna changamoto kubwa ya kufikiri na kuunda mustakabali tunaoutamani kwa Afrika na kwa dunia. Njia pekee zinanazoweza kutufikisha zitakuwa zile ambazo, kimsingi, zitazingatia ujasiri, uhuru na ukweli – vitu ambavyo vita vyake kamwe havimaliziki – kwa moyo wa kuunda mafungamano mapya ya kijamii.

Katika muktadha wetu wa sasa wa mapinduzi makubwa ya kiteknolojia na kidijitali, wanadamu hawajawahi kuwa na fursa nyingi kama walizonazo leo ambazo zinazoweza kubadilisha kabisa hali na namna ya maisha ya wanaume na wanawake. Aidha, hatujawahi kukaribia kuvuka mipaka yote iliyopo kama tulivyo sasa. Umakini endelevu utakaotuwezesha kuzielewa fursa na changamoto hizi, pamoja na nafasi husika katika kusukuma mustakabali wa bara hili unahitajika – yaani kuelewa na kutafsiri matarajio ya watu, kwa makundi, na kwa watu binafsi walio barani pamoja wa wale walio ughaibuni, mbali na kusimbua ubunifu wa maisha yao ya kila siku - ni miongoni mwa tezo muhimu zilizotuhamasisha kuzindua jarida hili la *Global Africa*.

Mradi huu wa kimataifa unaoujumuisha na kuangazia taaluma anuwai maskani na makutano yake ni Afrika inapoingiliana na dunia, ni matokeo chanya ya miradi ya muda mrefu ya tafakuri na ubadilishanaji wa ujuzi, yenye lengo la kuihuisha Afrika na maarifa ya Kiafrika. Hivyo, chanzo cha kuzinduliwa kwake ni hayo matunda ya mikutano mingi iliyojaa furaha, mijadala kinzani juu y dhima na nafasi ya utafiti na maarifa katika kutafuta majibu ya changamoto za Kiafrika na za kimataifa. Zaidi ya hayo, ni zao la kujiuliza maswali ya msingi kuhusu mitazamo yetu, kulingana na jinsi tunavyoyachukulia na kuyaelewa masuala hayo: *fikira*

This is an Open Access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution License CC-BY (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0), which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium, except for commercial purposes, provided the original work is properly cited.

tunduizi inachangia kuimarisha misingi ya kiepistemolojia, kinadharia, kimethodolojia na ki*deontolojia* juu ya tafiti zinazofanywa na Waafrika/na za Kiafrika, na juu ya mazingira ya majadiliano yaliyo huru kikweli katika Bara hili na duniani kote.

Waanzilishi wake walikuwa na nia ya dhati ya kuidhibiti baadhi ya migongano ya kijiografia, kiisimu, kitaaluma, na kiitikadi ambayo imelizuia au kulibabaisha bara la Afrika katika jitihada za kuondosha mifumo na mienendo ya ukandamizaji ambayo kwa muda mrefu imeyadhoofisha mahusiano kati ya Afrika na dunia, na kama dhihaka kuiathiri Afrika yenyewe pasipo yenyewe kujitambua.

Kwenye uwanja ambao kanuni za ushirikiano wa masuala ya kisomi zitawekwa, ikitambuliwa pia kwamba kuna mapungufu ya ujuzi na kuwa patakuwa na kutegemeana – zinageuka na kuwa nguzo kuu za kuzalisha kwa pamoja kwa ujuzi na maarifa ya kitaaluma, hivyo *Global Africa* inategemea kuwa na sera ya uwazi kwa:

– kukaribisha michango kutoka kwa wote, bila ya kujali fani au silsila zao; watafiti wachanga/wanaochipukia watapewa kipaumbele;

– kukaribisha michango inayochambua mada zilizo muhimu kwa bara la Afrika, na ambazo dhana/ruwaza zake kuu zitatathminiwa upya;

– kukaribisha sanaa na maarifa asilia;

– kuwakaribisha watumiaji wa maarifa yaliyozalishwa (watendaji wa asasi za kiraia, wanaharakati wa kisiasa, watoa maamuzi, sekta binafsi, pamoja na wananchi)

– la mwisho, kukaribisha lugha za Afrika zikihamasishwa kuwa lugha za utafiti na za kazi. Kwa hivyo, jarida linarasimisha lugha za Kifaranza, Kiingereza, Kiarabu, na Kiswahili (tunatumai kutumia lugha nyingine za Afrika pia zitaingizwa baada ya muda si mrefu) zitakuwa lugha za machapisho, jambo ambalo litachangia kumaliza utengano katika nyanja za kitaaluma.

Global Africa inaamini fursa hizi zitapata uhalali mkubwa endapo zitajikita zaidi kwenye maarifa yatakayozalishwa hapa na kuthibitishwa kupitia viwango bora vya kitaaluma. Ili kuimarisha mfumo ikolojia wa uchapishaji wa maarifa ya kisayansi barani Afrika, maandishi yatakayochapishwa na *Global Africa* yatatii sharti kuu: kuwekeza katika masomo ambayo yanakuza maarifa, uelewa wa uhalisia, katika nyanja mbalimbali– ziwe za kitaaluma au za kuchambua mada - kulingana na miundo mahususi ya kinadharia na dhana, pamoja na data thabiti zilizothibitishwa.

Kwa kufanya hivyo, tunatafuta kurekebisha upuuzwaji wa tafiti na machapisho ya Kiafrika katika medani ya kimataifa, ingawa bara hili ni sehemu ya kupigiwa mfano kwa maingiliano yake kwenye masuala ya ndani, ya kitaifa, ya jamii na ya kimataifa – kupitia ubunifu na mivutano inayotambulika. Matarajio kama haya yanatupasa kuunda uwanja wa uweledi na nidhamu ambapo sauti za watafiti wa Kiafrika zitasikika, na utakaokaribisha kazi zote za utafiti ambazo zinachangia katika kuitafakari upya Afrika na ulimwengu kupitia mtazamo wa Kiafrika ili kuelezea na kubuni mapitio yake.

Global Africa inadhamiria kuwa jumuiya ya Afrika nzima yenye kunawiri na matumaini, inayomkaribisha yeyote anayetaka kuishi katika eneo ambalo si kwamba halina masharti, lakini hapa hawatapoteza mtima wao. Tukiwa tumejizatiti kwa matumaini hayo, tungependa kuiunda karne ijayo, kwanza na kabla ya yote, kwa kusikiliza sauti na mitetemo ya vijana wasomi wa bara hili na wale waliopo diaspora.